*Mwanamke akikataa kuwa Hateswi:*

- Mhakikishie kuwa anaweza kuzungumza nawe wakati wowote.
- Usimkasirikie wala uamuzi wake usikuvunje moyo. Ni muhimu kuelewa kuwa ana uoga au hayuko tayari kuchukua hatua zingine.
- Jaribu kuelewa ni kwa nini mwanamke anasita kuomba msaada. Anaweza kuona haya.
- Jitolee kwenda naye iwapo atahitaji habari zaidi au usaidizi.
- Kama ana watoto, mjulishe kwa upole kuwa unahusika na usalama wake na pia wa watoto wake. Anaweza kugundua kuwa hali yake si nzuri akifahamu kuwa watoto wake wanaweza kuwa hatarini pia.

*Haya ni baadhi ya mambo ya Kufikiria kuhusu kusaidia:*

| Hoja ya Kuwaza | Hoja ya Kufikiria |
| --- | --- |
| Unajisikia kuwa hayakuhusu | Huenda ikawa ni hali ya kufa na kupona. Vurugu inahusisha kila mtu |
| Hujui la kusema | Ni vizuri ukisema kuwa unajali na unahusika |
| Unaona kama utaharibu mambo zaidi | Mambo huenda yakawa mabaya zaidi iwapo hutafanya chochote |
| Mambo si mabaya sana yakuweza kuwahusisha polisi | Polisi wana mafunzo na njia za kutoa huduma |
| Unaogopa kuwa mwanaume atakudhuru wewe au familia yako | Muongeleze mwanamke akiwa peke yake. Wajulishe polisi kama ukitishwa |

